

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA THELATHINI

16 MEI, 2018



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA THELATHINI- TAREHE 16 MEI, 2018

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

251. MHESHIMIWA RESTITUTA TASKA MBOGO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Wabunge wa Viti Maalum ni sawa na Wabunge wengine wa Majimbo kwa

sababu hakuna tofauti ya kiapo cha Wabunge wa Majimbo na wale wa Viti Maalum:-

Je, ni kwa nini Wabunge wa Viti Maalum hawaingii kwenye Vikao vya Kamati za Fedha za Halmashauri zao.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

252. MHESHIMIWA BUPE NELSON MWAKANG'ATA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Wanawake ni nguzo muhimu katika kukuza uchumi na kusimamia nchi yetu na kwamba ukimwezesha Mwanamke umeiwezesha familia na Taifa kwa ujumla:-

Je, ni lini Serikali itafikiria kuboresha huduma za kibenki zitakazoweza kuwahudumia akina mama walio Mikoa ya pembezoni.

253. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (B.L.W):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Katika utekelezaji wa Bajeti ya 2017/2018 Serikali imekuwa ikitegemea msaada wa wafadhili 'Basket Fund' ili kutunisha Mfuko

wa Hazina katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Maendeleo:-

- (a) Je, ni kiasi gani cha fedha kutoka *'Basket Fund'* kimepatikana katika Mwaka 2017/2018;
- (b) Je, kati ya fedha hizo ni kiasi gani kimepelekwa Zanzibar kusaidia Bajeti.

WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

254. MHESHIMIWA ALLY SALEH ALLY (MALINDI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:- Utaratibu wa kutunga Sheria wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unahusisha maslahi ya nchi zote tano wanachama wa EAC kuelekea fungamano la kiuchumi na kisiasa:-

- (a) Je, hadi sasa ni Sheria ngapi zimeshatungwa na kwa mgao wa maeneo yapi;
- (b) Je, hatua gani huchukuliwa unapotokea mgongano baina ya Sheria ya ndani na ile ya Jumuiya;

(c) Je, kuna utaratibu gani wa kutoa elimu ya umma kuhusu Sheria za Jumuiya.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

255. MHESHIMIWA GODBLESS JONATHAN LEMA (ARUSHA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara ya mzunguko wa Afrika Mashariki (*By pass*) inayojengwa katika Jiji la Arusha na viunga vyake inaonekana kusuasua ingawa fedha za ujenzi zimeshapatikana:-

Je, ni lini Serikali italipa fidia kwa Wananchi walioacha maeneo yao kwa ajili ya mradi huo.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

256. MHESHIMIWA MARYAM SALUM MSABAHA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Bagamoyo ni Mji Mkongwe wenye vivutio

vya kitalii kama ilivyo Miji mingine nchini kama vile Zanzibar, Kilwa na Tanga:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha vituo vya kitalii nchini ikiwemo Bagamoyo ili kupata wageni wengi na kukuza pato la Taifa.

257. MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA (VITI-MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Serikali hupeleka katika Halmashauri zilizopo katika Hifadhi ya Wanyamapori asilimia 25 ya fedha zitokanazo na mapato ya uwindaji wa Kitalii na upigaji picha pasipo Halmashauri husika kujua msingi wa tozo hizo:-

- (a) Je, ni lini Serikali itaanza kupeleka takwimu ya mapato yanayopatikana ili Halmashauri ziweze kujua stahiki zake;
- (b) Je, ni kiasi gani cha mapato kimepatikana kutokana na Maswa Game Reserve na Hifadhi ya Makao na kiasi gani kilipelekwa katika Wilaya ya Meatu kila mwaka kuanzia mwaka 2015 hadi 2017.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

258. MHESHIMIWA MOHAMED OMARY MCHENGERWA (RUFJI):


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:- Wananchi wa Kata za Mwaseni, Mloka, Ngoroko na Kipungila Wilayani Rufiji waliruhusiwa kuingia ndani ya Hifadhi ya Selous na kuvua Samaki na hivyo kuinuka kiuchumi. Baada ya marekebisho ya mipaka ya Hifadhi wananchi wamezuiwa kuingia kwenye Hifadhi na wakati mwingine wanatendewa vitendo kinyume na sheria:-

- (a) Je, Serikali inachukua hatua gani kusaidia wananchi wa maeneo hayo ili waweze kupata kipato;
- (b) Je, Serikali inachukua hatua gani kurejesha amani kati ya Vijiji vinavyozunguka maeneo ya mipaka ya Hifadhi na watumishi wa Hifadhi.

WIZARA YA NISHATI:

259. MHESHIMIWA ISSA ALI MANGUNGU (MBAGALA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

- 
- (a) Je, ni lini ujenzi wa Kituo kidogo cha kupoza umeme “*substation*” ya Mbagala utakamilika;
- (b) Je, makubaliano ya mkataba wa ujenzi wa Kituo hicho ulikuwa wa muda gani;
- (c) Je, Mkandarasi wa mradi huo yupo ndani ya muda au amecheleweshwa kazi kwa mujibu wa Mkataba, na je ni hatua gani zimechukuliwa.

260. MHESHIMIWA JUSTIN JOSEPH MONKO (SINGIDA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Mradi wa REA Awamu ya II katika Jimbo la Singida Kaskazini ulisimama tangu mwaka 2016 na kukosesha huduma hiyo kwa vijiji vilivyokusudiwa mwaka 2017, utekelezaji wa REA Awamu ya III katika vijiji 30 kati ya 64 vilivyokusudiwa umeanza:-

- (a) Je, ni nini kauli ya Serikali juu ya ukamilishaji wa mradi wa REA II;
- (b) Je, ni lini mkandarasi wa REA III awamu ya pili atapatikana na kuanza kazi.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA KILIMO:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

(Majadiliano yanaendelea)

DODOMA
16 MEI, 2018

S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE